**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Simu Na. +255 026 2702191
+255 026 2702715
Fax Na. +255 026 2702082
**Barua pepe: ras@iringa.go.tz**
**Tovuti: http://www.iringa.go.tz**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
4 Barabara ya Pawaga,
Mtaa wa Gangilonga,
S.L.P. 858,
**51108, IRINGA.**

**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb. FA.255/265/01J/139**

**16 Januari, 2025**

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Manispaa,
**Iringa.**

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji,
**Mafinga.**

Wakurugenzi Watendaji,
Halmashauri za Wilaya,
**Iringa, Kilolo na Mufindi**

Kun: **KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI KUHUSU "EFFECTIVENESS OF PRODUCTIVE SOCIAL SAFETY NETS ON BENEFICIARY HOUSEHOLDS' GRADUATION INTO SUSTAINABLE LIVELIHOODS"**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imepokea barua yenye Kumb Na. **AB.307/323/01/07** kutoka OR– TAMISEMI na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), kuhusu kibali cha kufanya utafiti kilichotolewa kwa **Bw. Jonas Charles**.

3. Muda wa kufanya utafiti huu ni tarehe 15 Januari hadi 15 Juni, 2025. Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali itafanya ukaguzi wakati wowote kujiridhisha na utekelezaji sahihi wa kibali hiki.

4. Takwimu zitakazokusanywa kutokana na utafiti huu ni kwa ajili ya matumizi ya ndani tu na iwapo zitatakiwa kuchapishwa na kusambazwa kibali kutoka Mamlaka husika kitapaswa kuombwa.

5. Kwa barua hii, unaombwa kumpokea na kumpa ushirikiano utakaohitajika kwa ajili ya kukamilisha utafiti huu kama ulivyokusudiwa.

=== Nashukuru kwa ushirikiano wako.

Doris N.Kalasa
**KATIBU TAWALA MKOA**

OnlinePhotoScanner.com

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI**

*Unapojibu tafadhali taja;*

**Kumb. Na. HW/MUF/S.40/43 VOL.IV/42** **29/01/2025**

Mtendaji wa Kijiji,
Kijiji cha Idetero, Lugodalutali, Nyololo Njiapanda, Ikongosi,
Ikimilinzowo, Luhunga na Mninga,
**MUFINDI.**

Kuh: **KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI KUHUSU "EFFECTIVENESS OF PRODUCTIVE SOCIAL SAFETY NETS ON BENEFICIALY HOUSEHOLDS" GRADUATION INTO SUSTAINABLE LIVELIHOODS"**

Tafdhali husika na somo tajwa hapo juu,

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imepokea barua yenye Kumb. **Na.FA.255/265/01J/139** ya tarehe **16 Januari, 2025** kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa inayohusu Kibali cha kufanya utafiti kuhusu "effectiveness of productive social safety nets on beneficialy households" graduation into sustainable livelihoods"

3. Kwa barua hii, nakujulisha kuwa zoezi hili litafanywa na mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine katika Wilaya ya Mufindi kwa Kata za (i) Mbalamaziwa kijiji cha Idetero, (ii) Igombavanu kijiji cha Lugodalutali, (iii) Nyololo kijiji cha Nyololo Njiapanda, (iv) Ikongosi kijiji cha Ikongosi, (v)Itandula kijiji cha Ikimilinzowo, (vi) Luhunga kijiji cha Luhunga na kata ya Mninga kijiji cha Mninga. Aidha zoezi hili litafanyika kuanzia tarehe 15 Januari hadi 15 Juni, 2025.

4. Natumaini kuwa utawapatia ushirikiano wa kutosha kwa kuzingatia sheria, Kanuni na Taratibu za miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma.

Sigifridi A. Kaunara
Kny: **MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**MUFINDI**

**NAKALA**: Mkurugenzi Mtendaji (W) - Aione kwenye jalada

Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) - Kwa taarifa



OnlinePhotoScanner.com